# KCSE ISIMU JAMII

# QUICK REVISION

***1st Series of Possible Testable KCSE Questions***

## (TRIALS 1-50)

## *A PREDICTION OF EXPECTED KCSE QUESTIONS*

***For Marking Schemes, Call/WhatsApp 0746 222 000***

**MWALIMU AGENCY**

# KCSE ISIMU JAMII 1

**1.** Saidi : Hallo...........Hallo....Huyo ni Bw. Mohamed?

Mohamed : Ndio...uko wapi...

Saidi : Shuleni...sasa...ulinifikishia ujumbe?

Mohamed : La. Parade ilikuwa imehitimishwa

Saidi : Sina credit. Nipigie tafadhali.

Mohamed : Sina pia, nitatuma sms

Saidi : Iwe saa hii eh?

Mohamed : Baada ya dakika tano

Saidi : Good day

Mohamed : Welcome

**(a)** Taja na uthibitishe sifa zinazojitokeza katika mazungumzo haya

**(b)** Eleza sababu za wazungumzaji kutumiambinu zifuatazo katika mazungumzo yao

(i) Mdokezo

(ii) Lugha mseto

# KCSE ISIMU JAMII 2

**2 .** Lugha ya kiswahili inakabiliwa na matatizo mengi sana. Yataje na kuyaeleza.

# KCSE ISIMU JAMII 3

**3.** ***Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali yanayofuata:-***

Uchunguzi uliofanywa umeonyesha kuwa anasumbuliwa na uto mwingi mwilini. Uto unaweza kudondoshwa kwa kufanya mazoezi, kupunguza ulaji wa vyakula vya wanga na hata protini. Protini iwapo nyingi mwilini hugeuzwa kuwa glukosi ambayo huhifadhiwa mwilini. Hii huwa msingi wa unene pia ambao unahatarisha

afya. Jamaa yake aliyeaga dunia alikuwa mgonjwa wa bolisukari ambayo inaweza kurithishwa. Kimsingi, lazima awe na welewa bora kabisa wa lishe. Mwenzake naye aliathiriwa na **aflatoxins** zilikuwa kwenye chakula alichokula.

**(a)** Sajili hii inapatikana wapi? Kwa nini?

**(b)** Taja sifa zinazohusishwa na sajili yenyewe

# KCSE ISIMU JAMII 4

**4.** Fafanua mikakati mitano inayoweza kuchapuza kukua na kuenea kwa kiswahili nchini Kenya

# KCSE ISIMU JAMII 5

**5** (a) Ni mambo yapi yanayochangia kudidimia kwa Kiswahili nchini Kenya.

(b) Mambo haya yanaweza tatuliwa vipi?

# KCSE ISIMU JAMII 6

**6.** a) Bainisha kwa kutoa mifano sifa **tano** za lugha ya vijana '**sheng'**

b) Fafanua changamoto **tano** zinazozuia maenezi ya haraka ya lugha ya Kiswahili

# KCSE ISIMU JAMII 7

**7.** ***Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali yanayofuata:-***

Niaje wasee! Ma-holiday ndizo hizo tena. Najua ma-mission ni mingi! Lakini jo, mambo imebadilika ! Ni kubaya maze. Usifikirie kila kitu unaona ni reality, ukadhani ni gold !

Hiyo siyo real life maze ! Round hii maze ni ''Ku-chill!'' Usipige ma-stunts zingine zitakuacha uki-regret later! NI POA KU- CHILL au aje maze?

a) Bainisha rejista ya mazungumzo haya

b) Kwa kurejelea kifungu andika sifa za rejista hii.

c) Kwa nini watu hutumia lugha zaidi ya moja.

d) Orodhesha hatua tatu zinazoweza kuchukuliwa kusuluhisha matatizo yanayokumba Kiswahili nchini.

# KCSE ISIMU JAMII 8

8. ***Soma mzungumzo yafuatayo kisha ujibu maswali :***

**A** : Ohh, dada Naomi

**B** : Dada Ruth (anamsogea kwa bashasha wanakumbatiana). Ahh Mungu asifiwe!

**A**: Asifiwe sana

**B**: Ehh dadangu, miezi ...mingi...sijakuona

**A**: dada wee...Nilitumwa huko kusini ...Kuwahubiria watu injili (mtuo mdogo)singeweza kukata...

**B**: Ehh, usiwe kama Yona

**A**: Habari ya siku nyingi?

**B**; Nzuri Mungu bado ameendelea kunibariki

**A**: Amen!

**B**: Nimeendelea kuiona neema yake

**A**: Amen! Asifiwe Bwana

**B**: Halleluya

**A**: Ni Mungu wa miujiza!

**B** : Amen. Hata nami nimeona neema yake

Bado niko imara katika wokovu katika siku hizi za mwisho

**A** : Amen !

**B** : Ni Mungu wa ajabu kweli !

**A** : Nilikumbana na matatizo lakini nikategemea sala

Kama Paulo na sila… Na nikashinda (anatua). Sikuweza kumpa shetani nafasi…maana ameshindwa

**B** : Ameshindwa kabisa

**Maswali**:-

(i) Hii ni sajili ya wapi ? Fafanua

(ii) Taja na ueleze sifa za sajili hii

(iii) Taja na ueleze mambo **mawili** muhimu yaliyosaidia katika maenezi ya Kiswahili Afrika mashariki na kati

# KCSE ISIMU JAMII 9

**9.** Bw. Mosuka : Mheshimiwa spika, naichukua fursa hii kuipinga hoja iliyowasilishwa na mbunge wa Mahira, mheshimiwa Kochaberi kuhusu suala la kuavya....

(a) Hii ni sajili gani?

(b) Eleza sifa za mazungumzo ya sajili hii

# KCSE ISIMU JAMII 10

**10.** Eleza juhudi tano zinazotumika kukiendeleza Kiswahili

# KCSE ISIMU JAMII 11

**11.`** (a) Fafanua sifa za matumizi ya lugha katika muktadha wa maabadini

(b) Matumizi ya lugha yoyote ile huthibitiwa na mambo fulani. Fafanua **matano** kati ya hayo

# KCSE ISIMU JAMII 12

**12.** **AZIZ** : Ingia 46! Adams mbao Kenyatta, railways beba! 46 Adams mbao kenyatta, railways!

**SHIKU** : Namba nane ngapi?

**AZIZ** : Mbao ingia, blue.

**SHIKU** : Nina hashuu.

**AZIZ** : Blue Auntie.

**SHIKU** : Sina.

**AZIZ** **:** Ingia. 46 Adams mbao, kenyatta railways gari bebabeba.

**AHENDERA** : Mimi sinako shirini. Chukuako tu kumi.

**AZIZ** : Dinga inakunywanga petrol mzee.

**AHENDERA**: Kumi mingi.

**AZIZ** : Haaya ingia twende. Driver imeshon twende.

**Maswali**

(i) Eleza muktadha wa mazungumzo haya

(ii) Taja sifa **sita** za lugha iliyotumika katika mazungumzo haya

# KCSE ISIMU JAMII 13

**13.** ***Kifuatacho ni kifungu kifupi cha mazungumzo. Kisome kisha ujibu maswali yaliyoulizwa:-***

Mzee Oluoch : ...............................................................ni kweli hayo!

Mzee Mwenda : Ndio. Huyu mtoto wangu nimemsomesha mpaka akahitimu chuo kikuu na anafanya kazi ya uhasibu.

Mzee Oluoch : Na wangu amehitimu na sasa ana shahada ya uzamili. Yeye ni mhandisi mkuu. Chukua tu mbuzi hamsini na utukubalie kujenga uhusiano wa ukwe.

Mzee Mwenda : Je, mbuzi hao ni wa 'mfuko' au ni .......?

Mzee Oluoch : Kuna wa mfuko ......thelathini na hao wengine ishirini.

Mzee Mwenda : Basi lete hao ulio nao. Wengine hamsini watabaki deni. Utakuwa ukinilipa polepole. Idhini yangu nimetoa ili mipango iendelee.

(a) Mazungumzo ya aina hii hutokea katika muktadha wa aina gani?

(b) Eleza sifa **nane** za lugha inayotumika katika wa aina hii

# KCSE ISIMU JAMII 14

MTU 1: Una shida gani?

MTU 2: Kichwa chaniwanga, tumbo lanisokota na ninahisi uchovu mwingi. Nisaidie tafadhali.

MTU 1: Pole, afya yako itakuwa shwari. Hizi tembe hapa zitakusaidia kupunguza maumivu. Unapaswa kuzitumia mara tatu kwa siku…

**(a) (i)** Tambua sajili hii **( alama 2)**

**(i)** Kwa kutolea mfano, andika sifa tatu ambazo zingetumika katika sajili hii **( alama 3)**

**(b)** Umepewa jukumu la kuendesha shughuli ya mazishi kijijini mwako. Fafanua sifa tano za lugha utakayotumia wewe na waombolezaji wengine. **(alama 5)**

# KCSE ISIMU JAMII 15

**4. <u>ISIMUJAMII:</u>** **(alama 10)**

Nipe chai, andazi mbili na egg moja…………

a) Taja sajili inayorejelewa na maneno haya **(alama 2)**

b) Fafanua sifa nne zinazohusishwa na sajili hiyo **(alama 8)**

# KCSE ISIMU JAMII 16

**a)** Eleza maana ya usanifishaji wa lugha. **(alama 2)**

**b)** Taja lahaja zozote mbili za kati. **(alama 2)**

**a)** Kulingana na habari zinazotufikia hivi punde, maafisa watatu wa polisi jana walikana mashtaka ya mshukiwa wa mauaji ya watoto 13 kutoroka kutoka kituo cha polisi.

i) Tambua sajili inayorejelewa. **(alama 1)**

ii) Eleza sifa **tano** za sajili hii. **(alama 5)**

# KCSE ISIMU JAMII 17

**ISIMU JAMII** **(Alama 10)**

**a.** Eleza nadharia tatu kuhusu chimbuko la Kiswahili. **(alama6)**

**b.** Fafanua istilahi zifuatazo: **(alama 4)**

**i.** UwiliLugha

**ii.** LinguaFranka

**iii.** Misimu

**iv.** Sajili …

# KCSE ISIMU JAMII 18

**ISIMUJAMII**

**1.** Taja na ufafanue nadharia tatu zinazoelezea asili ya lugha ya Kiswahili

**(Alama 6)**

**2.** Eleza maana ya istilahi zifuatazo za isimujamii

(a) Lafudhi **(Alama 2)**

(b) Rejesta **(Alama 2)**

# KCSE ISIMU JAMII 19

**4. ISIMU JAMII (ALAMA 10)**

**i)** Soma makala yafuatayo kisha ujibu maswali.

Ahabu: Likizo ilikuwa fupi tumerudi kwa vitabu sasa.

Munini: Huu ni wakati wa kipindi cha lala salama, lazima tujikaze.

Ahabu : Usemavyo ni real.

Munini: Bidii ndiyo itakayotuokoa.

Ahabu : Ulimaliza ile assignment. Maze mimi nilishindwa.

Munini: Shsss… ndo huyo mwalimu.

Bw. Juma: Nani hao wanaongea? Nyamazeni! Tumekuja hapa kusoma sio kupiga kelele.

**MASWALI**

**a)** Tambua sajili inayorejelewa katika kifungu hiki. **(alama 1)**

**b)** Fafanua sifa nne za sajili hii kama zilivyojitokeza katika kifungu **( alama 4)**

**ii)** Taja nadharia tatu zinazoeleza chimbuko la lugha ya Kiswahili. **( alama 3)**

**iii)** Eleza istilahi zifuatazo katika isimu jamii **(alama 2)**

**a)** Usanifishaji

**b)** Lafudhi

# KCSE ISIMU JAMII 20

**ISIMUJAMII** **(alama10)**

**(a)**Tofautisha kati ya kuhamisha msimbo na kuchanganya msimbo. **(alama 2)**

**(b)**Taja mambo mawili yanayochangia katika uhamishaji msimbo. **(alama 2)**

**(c )**Taja kaida mbili zinazotawala maamkizi katika jamii huku ukitoa mifano mwafaka. **(alama2)**

**(d)** Fananisha sifa zozote nne za sajili ya maabadini na mahakamani. **(alama 4)**

# KCSE ISIMU JAMII 21

**4. ISIMU JAMII *(alama10*)**

1. "Mheshimiwa spika naomba nipewe fursa kutoa maoni yangu kuhusu hoja iliyowasilishwa…"

**(a)** Weka makala haya katika muktadha wake. **(Alama 2)**

**(b)** Eleza sifa za mazungumzo yanayofanywa katika muktadha huo uliotajwa. **(Alama 8)**

# KCSE ISIMU JAMII 22

**4. ISIMU JAMII (ala 10)**

"Chenga chenga, chenga tena, aaaa baas! Goal! Habari ndio hiyo ndugu yangu!

(a) Tambua sajili hii. **(ala 2)**

(b) Huku ukitoa mifano, eleza sifa bainifu za sajili uliyotaja hapo juu. **(ala 8)**

# KCSE ISIMU JAMII 23

**ISIMU JAMII (ALAMA 10)**

(a) Eleza kwa ufupi jinsi mambo yafuatayo yanavyodhibiti mitindo ya lugha

(i) Mazingira **(alama 2)**

(ii) Mada **(alama 3)**

**(iii)** Hali **(alama 2)**

(b) Fafanua sera tatu ambazo zimepitishwa na serikali zinazochangia kuimarika kwa lugha ya Kiswahili**.** **(alama 3)**

# KCSE ISIMU JAMII 24

1. **ISIMU JAMII (ALAMA 10)**

**(a)** Eleza majukumu **matatu** ya lugha ya taifa. **(alama 3)**

**(b)** Fafanua mtindo wa lugha uliotumiwa katika taarifa ifuatayo huku ukieleza sababu za matumizi ya vitambulisho maalum vya lugha. **(alama 4)**

Wananchi, mimi sina mengi. Hapana katika nyinyi asiyenielewa. Sina la kusema, ila ninawakumbusheni kuwa mnahitaji kiongozi atakayeshughulikia maslahi ya taifa zima. Mtu huyo ni mimi na ninajitahidi niwezavyo kujenga masoko, barabara, shule zaidi na mazahanati na maisha yenu yatakuwa ya raha zaidi.

**(c)** Thibitisha kuwa adabu za lugha hazizingatiwi miongoni mwa wanajamii siku hizi. **(alama 3)**

# KCSE ISIMU JAMII 25

**ISIMU JAMII**

**a)** Eleza sababu zozote sita zinazochangia kufa kwa lugha. **(alama 6)**

**b)** Taja mambo yoyote manne yanayofanywa na serikali yetu kuimarisha lugha ya Kiswahili **(alama4)**

# KCSE ISIMU JAMII 26

**ISIMU JAMII**

**a)** Eleza sababu zozote sita zinazochangia kufa kwa lugha.

**(alama 6)**

**b)** Taja mambo yoyote manne yanayofanywa na serikali yetu kuimarisha lugha ya Kiswahili

**(alama4)**

# KCSE ISIMU JAMII 27

**ISIMU JAMII (Alama 10)**

**(a)** Eleza tofauti kati ya kuchanganya ndimi na kuhamisha ndimi. **(alama 2)**

**(b)** Andika sababu nne za kuchanganya na kuhamisha ndimi. **(alama 4)**

**(c)** Kiswahili ni lugha ya kibantu kulingana na ushahidi wa ki-isimu. Thibitisha kauli hii. **(alama 4)**

# KCSE ISIMU JAMII 28

**1. SEHEMU YA D: ISIMU JAMII (ALAMA 10)**

(a) Eleza mitazamo mine kuhusu chimbuko la Kiswahili.

**(alama 4)**

(b) Eleza njia za uundaji wa maneno katika lugha ya Kiswahili.

**(alama 6)**

# KCSE ISIMU JAMII 29

## SEHEMU YA D: ISIMU JAMII: (ALAMA 10)

**(a)** Ali: Wee kuja hapa. Wewe ni nani? Sema haraka!

Ebo: Mimi … ni … afande ni Ebo

Ali: Unatoka wapi sa ii? Hapa hakuna sheria?

Ebo: Samahani mkubwa. Mimi niku…

Ali: Mkubwa wa nani? Wakubwa wako ofisini.

Ebo: Pole mzee.

Ali: Mzee gani? Hii mtu lazima niiwekwa store. Yaani self-contained. Toa viatu.

Ebo: Tafadhali Bwana Askari, nilichelewa …

Ali: Mimi sitaki hadithi! Hizo pelekea nyanya yako, eh. Fanya haraka!

Ebo: Naomba mkubwa …

Ali: Hapa si kanisani. Unaomba! Hata …

Fafanua sifa tano za sajili hii. **(alama 5)**

(b) Eleza maana ya istilahi zifuatazo za isimu jamii. **(alama 5)**

**(i)** Lugha ya taifa.

**(ii)** Lugha ya ishara

**(iii)** Lugha mwiko

**(iv)** Sajili za lugha

**(v)** Uchanganyaji msimbo.

# KCSE ISIMU JAMII 30

**4.** **ISIMU JAMII**:

***Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali yanayofuata.***

"Ndugu na madada, sote tumealikwa katika karamu hii ya Bwana kabla ya kujongea mezani pake, Bwana. Pana haja ya kutakasa nyoyo zetu na kujutia madhambi yetu. Sisi sote ni watenda dhambi na inastahili kumwendea ili aweze kutuondolea madhambi yetu."

**Maswali**

(i) Weka maneno haya katika sajili yake. **(alama 2)**

(ii) Nini kimekufanya uchague sajili uliochagua katika swali (i). **(alama 1)**

(iii) Eleza sifa za matumizi lugha katika sajili hii. **(alama 7)**

# KCSE ISIMU JAMII 31

**ISIMU JAMII** **(Alama10)**

**c.** Eleza nadharia tatu kuhusu chimbuko la Kiswahili. **alama6)**

**d.** Fafanua istilahi zifuatazo: **(alama 4)**

- **i.** UwiliLugha
- **ii.** LinguaFranka
- **iii.** Misimu
- **iv.** Sajili

# KCSE ISIMU JAMII 32

**ISIMU JAMII: (ALAMA 10)**

**(a)** **(i)** Eleza maana ya krioli. **(alama 2)**

**(ii)** Eleza sifa zozote tatu za krioli. **(alama 3)**

**(b)** **(i)** Eleza maana ya Lingua Franka **(alama 2)**

**(ii)** Tambua sifa zozote tatu za Lingua Franka **(alama 3)**

# KCSE ISIMU JAMII 33

**ISIMU JAMII** ***(AL.10)***

***Soma makala haya kisha ujibu maswali.***

Kwani mnauza salamu? Sina *time ya kuwaste hapa*. *Am a busy person* leta *order* yako haraka... Nimesema samaki wa kupaka. Mimi ng'ombe na *chicken*.

***(a)*** Tambua sajili hii. **(al.1)**

***(b)*** Fafanua sifa **tisa** za sajili hii. **(al.9)**

# KCSE ISIMU JAMII 34

4. **ISIMU JAMII**

Fafanua mambo matano yaliyochangia kuenea kwa Kiswahili nchini kabla na baada ya uhuru.

# KCSE ISIMU JAMII 35

**4. ISIMU JAMII** **(Alama 10)**

**Maswali**

**a)** "........ unaweza kukata rufaa iwapo unaonelea kuwa umehiniwa **.........**"

**i)** Bainisha sajili ya mazungumzo haya**.** **(al.1)**

**ii)** Fafanua sifa za matumizi ya lugha katika muktadha huu. **(al.4)**

**b)** Jadili changamoto zinazokumba kuimarika kwa Kiswahili katika jamii ya sasa. **(al.5)**

# KCSE ISIMU JAMII 36

**4.ISIMU JAMII (ALAMA 10)**

**a)** Eleza maana ya lugha rasmi **(alama 2)**

**b)** Fafanua sifa zozote za lugha rasmi. **(alama 8)**

# KCSE ISIMU JAMII 37

**4. ISIMUJAMII** **(Alama10)**

***Soma makala yafuatayo kisha ujibu maswali.***

Niaje wasee! *Midterm* ilibamba lakini ilkua fupi sana, tumerudi *books*, huu ni mwaka wa mwisho tujikaze jo. Msifikirie hizo hepi zetu ni *reality, kuchill* ni jambo la maana jo! ama niaje *bro…hustle ni real*, bidii ndio itatuokoa

**(a)** Tambua sajili inayohusishwa na kifungu hiki **(alama2)**

**(b)** Eleza sifa zozote **nne** za kimtindo zinazojitokeza katika kifungu hiki. **(alama 4)**

**(c)** Eleza sababu **nne** zinazosababisha matumizi ya lugha ya aina hii. **(alama 4)**

# KCSE ISIMU JAMII 38

**4. ISIMUJAMII** **(Alama 10)**

**(a)** Lahaja huainishwa katika makundi **mawili**. Yataje **(alama 2)**

**(b)** Eleza sifa zozote **nne** za lugha ya taifa. **(alama 4)**

**(c)** Tolea ushahidi namna **nne** kwamba Kiswahili ni lugha ya kimataifa. **(alama 4)**

# KCSE ISIMU JAMII 39

**ISIMUJAMII** **(ALAMA 10)**

**(a)** Eleza sifa **tano** za lugha rasmi **(alama 5)**

**(b)** Eleza mambo **matano** yaliyochangia katika maenezi ya Kiswahili katika

**(alama 5)**

**(c)** Afrika Mashariki kabla ya uhuru

# KCSE ISIMU JAMII 40

4. **ISIMU JAMII** **(Alama 10)**

**(a)** Eleza namna kaida zifuazo zinavyoathiri matumizi ya lugha katika jamii **(alama 4 )**

***(i)*** uhusiano

***(ii)*** malezi

**(b)** Eleza majukumu **mawili** ya lugha ya Kiswahili kama lugha ya taifa katika nchi ya Kenya

**( alama2)**

**(c)**Taja sifa **nne** zinazotambulisha sajili ya hospitali

# KCSE ISIMU JAMII 41

**4. ISIMUJAMII** **(ALAMA 10)**

**a)** Kwa nini kulikuwa na haja ya kusanifisha lugha ya Kiswahili. Toa sababu tano. **(alama 5)**

**b)** **"**….sote tunajua kwamba ni kudura. Makiwa!"

**i.** Tambua sajili iliyotumika katika dondoo hili. **(alama 1)**

**ii.** Eleza sifa nne za sajili hiyo. **(alama 4)**

# KCSE ISIMU JAMII 42

**ISIMU JAMII**

**(a)** Kwa nini kulikuwa na haja ya kusanifisha Kiswahili? Toa sababu tano **(ala. 5)**

**(b)** Fafanua sifa za lugha ya kazi **(ala. 5)**

# KCSE ISIMU JAMII 43

C. **ISIMU JAMII**

**(a)** Kwa nini kulikuwa na haja ya kusanifisha Kiswahili? Toa sababu tano **(ala. 5)**

**(b)** Fafanua sifa za lugha ya kazi **(ala. 5)**

# KCSE ISIMU JAMII 44

**4.** **SEHEMU D: ISIMUJAMII** (Alama 10)

***Soma mazungumzo yafuatayo kisha ujibu maswali.***

Kibiko: Hujambo dada Cheupe?

Cheupe: (*Akikohoa*) Sijambo ndugu Kibiko.

Kibiko: Unaendelea namna gani?

Cheupe: *Niko poa* isipokuwa maumivu kidogo ya *chest.*

Kibiko: Usijali nitakupa *pain relievers* utakuwa sawa.

Cheupe: Asante sana, nashukuru.

**Maswali**

a) Eleza muktadha wa mazungumzo haya. **(ala. 2)**

b) Taja na ueleze sifa za lugha inayotumika katika mazungumzo haya. **(ala. 8)**

# KCSE ISIMU JAMII 45

**4. ISIMU JAMII**

"Anachukua mpira, kisigino anatuliza, kengeuka, kulia, kushoto, hesabu wa kwanza tesa wa pili,baki peke yake na goalkeeper.

**a)** Taja sajili inayorejelewa na maneno haya. **(alama 2)**

**b)** Fafanua sifa za sajili hii. **(alama 8)**

# KCSE ISIMU JAMII 46

**4. ISIMU JAMII (ALAMA 10)**

**a)** Taja mambo **matatu** yanayopelekea kufifia na kufa kwa lugha **(al. 3)**

**b)** Isimujamii ina umuhimu gani kwa mwanafunzi wa shule ya upili **(al. 4)**

**c)** Andika sifa **tatu** za lugha utakayotumia kuwatangazia watu kuhusu kinyang'anyiro cha soka **(al. 3)**

# KCSE ISIMU JAMII 47

**1. ISIMU JAMII**

**a)** Taja mambo manne yanayopelekea kufifia/kufa kwa lugha, **(alama 4)**

**b)** Soma makala yafuatayo kisha ujibu maswali yafuatayo

**................**napinga hoja iliyotolewa na waziri wa Finance ya kupiga marufuku matumizi ya plastic bags. Baada ya kumsikiza kwa makini, napenda kumkosoa kwa kudhihirisha kuwa**.................** kulingana na kifungu nambari **..................**

**i)** Bainisha sajili ya mazungumzo hayo. **(alama 2)**

**ii)** Huku ukitoa mifano mwafaka, eleza sifa nne za sajili hii kwa mujibu wa kifungu hiki.

# KCSE ISIMU JAMII 48

**4. ISIMU JAMII.** **(alama 10)**

**a)** Lugha ya Kiswahili inakabiliwa na matatizo mengi sana. Taja matano na kuyaeleza. **(alama 5)**

**b)** Fafanua mikakati mitano inayoweza kuchapuza kukua na kuenea kwa Kiswahili nchini Kenya. **(alama 5)**

# KCSE ISIMU JAMII 49

**ISIMU JAMII**

Nani kuku.....? Sosi poa leo ...... Mate ndo! ndo! ndo!. Ukimanga hii hutaona daktari kwa miaka kumi...... Ng'ombe je? nani? ......nani!... Ni wewe....... poa basi naja............

**a)** Ni sajili gani inayorejelewa hapo juu? **(alama 2)**

**b)** Andika sifa za sajili hii ukitoa mifano ndani na nje ya muktadha huu **(alama 8)**

# KCSE ISIMU JAMII 50

**ISIMU JAMII**

Nani kuku.....? Sosi poa leo ...... Mate ndo! ndo! ndo!. Ukimanga hii hutaona daktari kwa miaka kumi...... Ng'ombe je? nani? ......nani!... Ni wewe....... poa basi naja............

**a)** Ni sajili gani inayorejelewa hapo juu? **(alama 2)**

**b)** Andika sifa za sajili hii ukitoa mifano ndani na nje ya muktadha huu **(alama 8)**

……………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………
………………………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………
………………………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………
………………………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………

# THE END

mwalimuagency@gmail.com

# FOR THE FOLLOWING;

- ✓ ONLINE TUITION
- ✓ REVISION NOTES
- ✓ SCHEMES OF WORK
- ✓ SETBOOKS VIDEOS
- ✓ TERMLY EXAMS
- ✓ QUICK REVISION KITS
- ✓ KCSE TOPICALS
- ✓ KCSE PREMOCKS
- ✓ TOP SCHOOLS PREMOCKS
- ✓ JOINT PREMOCKS
- ✓ KCSE MOCKS
- ✓ TOP SCHOOLS MOCKS
- ✓ JOINT MOCKS
- ✓ KCSE POSTMOCKS
- ✓ TOP SCHOOLS PREDICTIONS
- ✓ KCSE PREDICTIONS
- ✓ KCSE REVEALED SETS

# CALL/TEXT 0746 222 000

## CALL/TEXT/WHATSAPP

# 0746 222 000

*mwalimuagency@gmail.com*

# THIS IS A PRODUCT OF MWALIMU AGENCY

# POWERED BY MR ISABOKE

## success